**TANGAZO**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# TANGAZO KWA WATUMISHI WOTE WALIOHAMISHWA NA KATIBU MKUU OFISI YA RAIS - TAMISEMI KUTOKA HALMASHAURI MOJA KWENDA HALMASHAURI NYINGINE LAKINI BADO MISHAHARA YAO HAIJAHAMISHWA KWENDA KWA WAAJIRI WAO WAPYA HADI KUFIKIA MWEZI OKTOBA, 2025

Ofisi ya Rais - TAMISEMI inawataarifu watumishi wote ambao walihamishwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI kutoka Halmashauri moja kwenda Halmashauri nyingine lakini bado mishahara yao haijahamishwa kwenda kwa waajiri wao wapya kuwa mnatakiwa kuwasilisha **barua zenu za uhamisho pamoja na Check Namba zenu** ili kuwezesha uhamisho wa mshahara kwenye mfumo. Barua hizo ziwasilishwe kwa **nakala laini "scanned PDF" isiyozidi KB 500 ikiwa imekamilika kwenye ukurasa mmoja** kabla ya tarehe **30/11/2025** kwenye **e mail maalumu ya ofisi ifuatayo;**

**uhamisho.mishahara@tamisemi.go.tz**

Tafadhali zingatieni muda uliopangwa wa kuwasilisha nyaraka hizo maana baada ya tarehe hiyo Ofisi ya Rais - TAMISEMI haitaendelea kufanya uhamisho wa mishahara kwa kutumia nakala ngumu. Uhamisho watatakiwa kuombwa kwenye mfumo wa **e uhamisho** na mishahara itakua inahamishwa moja kwa moja kwenye mfumo.

Nawatakia utekelezaji mwema

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais - TAMISEMI,
Mji wa Serikali – Mtumba,
S.L.P. 1923,
11 Novemba, 2025
DODOMA.

CS CamScanner